*Ukweli Hauna Kutu*

# Pambazuko

Toleo Namba 004 | Jumatatu Agosti 01-07, 2022

**Uk. 2 - Pongezi rubani wa Precision Air**



# Balozi wa Marekani anayependa ‘kujichanganya’

● *Rafiki mkubwa wa mama ntilie, wauza mihogo*

**Mdomo wa Mandonga zaidi ya ngumi zake Uk. 19**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

**Uk. 4 - Nani mkweli ongezeko la mishahara?**

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

# Pongezi rubani wa Precision Air

JULAI 27, mwaka huu – 2022 itabaki kuwa siku ya kukumbukwa kwa abiria na watumishi ndani ya ndege ya Kampuni ya Precision ambayo ilipata hitilafu ikiwa angani.

Ndege hiyo yenye namba PW 467 ikitokea Kahama, ikielekea Dar es Salaam kupitia Mwanza, ilizima injini baada ya takribani dakika 51 kuruka kutoka uwanja wa ndege wa Mwanza.

Hofu ilianza kutokea baada ya abiria mmoja, kijana wa kizungu, kuanza kupiga kelele, akiwaeleza wenzake waliokuwa wameketi jirani, kwamba injini imezima.

Baadaye abiria wengine waliingiwa hofu, huku baadhi wakisali, wakilia na wengine kuonekana wamejiinamia, huku wamefunika nyuso zao.

Baada ya abiria kuonekana 'wakipaniki' ndipo rubani wa ndege hiyo alitangaza kuwepo kwa hitilafu hiyo huku akieleza kwamba hali siyo ya kutisha sana.

Rubani wa ndege hiyo baadaye alisika akiwaeleza abiria wake – mmoja wao akiwa ni mhariri mkuu wa gazeti hili – Pambazuko, kwamba wasiwe na wasiwasi, kwani ndege ingetua salama katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA-JRO).

Baada ya tangazo hilo, abiria wengi walionekana kuwa watulivu, pamoja na kwamba waliendelea kusali, huku wengine wakijiinamia – wakiwa tayari wanasubiri heri ya usalama wa maisha yao.

Rubani aliendelea kuwakumbusha kuwa watulivu kwani ndege itatua salama KIA na kuwa hatua zote za tahadhari zimechukuliwa kuhakikisha usalama wa abiria na ndege.

Kama alivyoeleza rubani, ndege hiyo ilitua salama na abiria walipongeza hatua ya rubani huyo na wafanyakazi wenzake ambao waliendelea kuhimiza utulivu huku wakihakikishia usalama. Abiria walipiga kofi, vigelegele, na wengine wakikisika wakisema – "Aksante Mungu."

Katika mazingira yoyote, taarifa za ndege kupata hitilafu ikiwa angani, huleta hofu na simanzi kwa abiria na hata wafanyakazi wa ndege. Na hata kama watatulizwa kwa maneno gani, taarifa hizo hubaki kuwa hofu kwa wengi, kama siyo wote, lakini "tulizo" la rubani wa ndege hiyo lilikuwa faraja kwani lilibeba maneno yenye kuleta ujasiri na imani kwamba ndege itatua salama.

Pambazuko inatambua kuwa kuwatuliza abiria kunapokuwa na hitilafu ndani ya ndege, ni kazi ya marubani na wasaidizi wao, na kwamba ni moja ya majukumu yao wanayofunzwa, lakini linavyowasilishwa kwa abiria hutofautiana baina ya marubani. Huyu alisikika akiwa na mamlaka. Akiwasilisha taarifa yake kwa uhakika na sauti isiyokuwa na chembe ya hofu.

Ndiyo maana Pambazuko tunampongeza yeye pamoja na wafanyakazi wenzake, huku tukihimiza marubani wengine kutenda wanayopaswa kila kunapotokea lolote.




## NUKUU



*Siku hizi darasani siyo mahali pa kuongeza tamaa ya kusoma zaidi vitabu – ili kupata maarifa, bali chumba cha kutafuta mbuni za kushinda mitihani, basi – Prof. Chachage Seithy Chachage (Dar es Salaam - Oktoba 01, 2005)*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** na kutuma neno **"HABARI"** ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: **pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

# Nani mkweli ongezeko la mishahara?

**Na Plato Hekimachius**

ONGEZEKO la mshahara wa wafanyakazi Tanzania lililotangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan, limegeuka kuwa sakata sasa na kuleta mvutano kati ya serikali na wafanyakazi baada ya kubaini "ongezeko" lisilotarajiwa.

Maswali mengi sasa yanaibuliwa baada ya wafanyakazi kuona hali halisi ya ongezeko hilo kwenye karatasi za maslahi yao wanazopewa kila mwisho wa mwezi. Ongezeko hilo limezua tafrani.

Wengi wanajiuliza, je, nani anasema kweli kati ya Rais Samia na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa? Nani alidanganya au kudanganyika? Kwa nini vyama vya wafanyakazi siku hizi vinazungumza lugha ya kiserikali?

Kwa nini wafanyakazi ni wakali sana kwa serikali, lakini wanyonge mbele ya viongozi wao? Kwanini vyama karibu vyote vya wafanyakazi vimezama katika rushwa na ufisadi na serikali iko kimya?

Maswali hayo hayana majibu mepesi na bila majibu halisi, hali ya maslahi ya wafanyakazi itazidi kuwa mbaya zaidi.

Rais Samia alipoongelea "jambo letu" na wafanyakazi siku ya Mei Mosi, 2022 aliashiria habari njema. Baadaye ilitangazwa kuwa nyongeza ya asilimia 23.3 imeongezwa katika "jambo letu". Hapakuwa na maelezo ya ziada.

Maelezo ya ziada yanayotolewa sasa kuwa hicho kiwango kilikuwa kwa ajili ya kima cha chini yanaidhalilisha taasisi ya urais. Ili taasisi hiyo isafishike, inahitajika kafara ya haraka.

Wizara zinazohusika na suala hili katika ujumla wake, zinahitaji kuwajibika kwa sababu kama ufisadi unatawala ndani ya vyama vya wafanyakazi, taifa zima linaweza kuingia katika mgogoro mkubwa wa migomo isiyoisha.

Faida moja ya rushwa katika taifa ni pale inapozuia harakati za kweli za kudai haki katika taifa letu. Serikali nyingi za Afrika zimejifunza kuwa badala ya kutumia mabomu na risasi, zinatumia rushwa kuwanunua viongozi wa harakati za kudai haki na hali bora kazini.


*Rais Samia Suluhu Hassan,*

Kimsingi, kitendo cha Waziri Mkuu Majaliwa kujitokeza na kutoa ufafanuzi, kumezua maswali mengi zaidi juu ya nyongeza ya mishahara. Kimeiweka serikali katika mizani ya kuonekana haikuwa wazi, hivyo kudhaniwa kuwaudhi zaidi wafanyakazi.

Ikumbukwe kwamba, wakati ongezeko hilo linatangazwa, wafanyakazi wa Tanzania hawakuonja ongezeko lolote la mishahara yao kwa miaka sita.

# Maswali yaibuka uteuzi wa Samia

**Na Mwandishi Wetu**

"HIVI tumeishiwa watu wa kuwa viongozi nchi hii? Hili ni swali lililosikika kwa wengi baada ya wiki iliyopita Rais Samia Suluhu Hassan kufanya uteuzi wa wakuu wa mikoa "wapya."

Ni mjadala ambao unaendelea kwenye mitandao mingi ya kijamii; Twitter, Facebook and hata makundi sogozi ya WhatsApp.

Ni swali linaloulizwa bila kutaka kuingilia mamlaka ya uteuzi ya rais,



*Halima Dendego*

lakini lenye mantiki ya kuhoji kwamba iweje sura zilezile zilizozoeleka ziendelee kupata fursa za kuongoza kana kwamba hakuna wengine wenye kuweza kuteuliwa?

"Hivi kweli mama (Rais Samia) amekosa sura zingine zenye uwezo wa kumsaidia kazi? Naona watu walewale tu, tena wengine wakithibitika kuharibu kazi huko walikokuwa awali, sidhani kama ni sahihi, kurudia sura zilezile," anaandika Manoni Kamango kwenye ukurasa wake wa Twitter.

Hata hivyo, mwingine akijiita Wa-Kulungwa, kwenye mtandao huohuo anaandika akisifia baadhi ya wateuliwa ambao anasema walitolewa kwa hila kwenye nafasi zao na kiongozi aliyepita, Rais John Magufuli.

Wa-Kulungwa anawataja wale anaodai walioondolewa kwa hila licha ya kufanya kazi nzuri kuwa ni pamoja na Halima Dendego – ambaye anakwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa. Hata hivyo hakueleza hila gani ziliwaondoa.

Mbali ya wakuu wa mikoa, Pambazuko limebaini kuwa Rais Samia amerejesha na "kutema" baadhi ya watendaji waliokuwa kwenye uongozi wa Magufuli ili kumsaidia kazi. Samia alikuwa Makamu wa Rais wa Tanzania wakati huo.

Miongoni mwa mawaziri waliorudishwa kwenye nafasi ni pamoja na Balozi Pindi Chana, ambaye amepewa Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika uongozi wa Magufuli, waziri huyu alianza kupotea kwenye ramani za siasa na uteuzi.

Aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi ambaye wakati wa utawala wa Magufuli, alionekana kuaminika na kuwa na nguvu zaidi – huku baadhi ya wakubwa wenzake wakimtaja kuwa; "naibu rais", lakini naye kwa sasa amebaki na ubunge na 'kazi maalum,'

Mawaziri wengine ambao walikuwa nje wakati wa Magufuli na kurejeshwa ni Nape Nnauye ambaye kwa sasa ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Nape wakati wa hayati Magufuli alifutwa kazi akiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutokana na kupingana na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na ambaye kwa utawala huo alikuwa akionekana kama mtoto wa Rais Magufuli kutokana na kutetewa karibu kwa kila jambo. Makonda anadaiwa ndiye 'aliyemchongea' Nape kwa Magufuli.

Kigogo mwingine ni Profesa Makame Mbarawa, ambaye alikuwepo kwenye uwaziri katika miaka mitano ya kwanza ya Magufuli ila aliachwa hadi Rais Samia alipomteua kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

## Kulala ni Sh. bilioni 12



MATAJIRI zaidi duniani hivi karibuni wataweza kupata starehe “za kufa mtu,” kwa kulipa Sh. bilioni 12 – kwa usiku mmoja wakiwa kwenye sayari ya Mars.

Hoteli yenye vyumba 12 tu, inayotajwa kuwa na starehe za kila aina, itaanza kujengwa hivi karibuni katika sayari ya Mars na kwamba inamilikiwa na tajiri namba moja duniai, Elon Musk.

Taarifa zinaeleza kuwa Musk ameamua kuwapa matajiri raha zaidi nje ya dunia na kwamba itakapokamika itakuwa na “starehe isiyopatikana mahali popote duniani.”

Hata hivyo, taarifa haziko wazi kwamba itakuwa na vitu gani vyenye starehe, ingawa inaelezwa kuwa na vitu vya thamani vilivyotumika kutengeneza samani zake ikiwamo dhahabu, almasi na vito vingine kila mahali.

**Mashirika**

## Kila dakika 2 binti anapata Ukimwi

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughukia Ukimwi (Unaids) limeeleza kuwa kwa kila dakika mbili zinazopita, binti anaambukizwa Ukimwi.

Taarifa ya Unaids, imebaini kuwa kwa mwaka jana- 2021, mabinti, wengi wakiwa na umri wa kati ya miaka 15-23, waliambukizwa ugonjwa huo, wengi wakiwa kutoka Afrika.

Sababu ya hali hiyo ni kurubuniwa kirahisi na wanaume, kutokuwa na elimu ya kutosha ya ugonjwa huo na wengine ni katika kujaribu uhusiano wa kingono.

**-AFP**

## Waziri jela kwa ufisadi

VITA dhidi ya rushwa nchini Msumbiji sasa imepamba moto baada ya waziri wa kazi wa nchi hiyo kuhukumiwa kifungo cha miaka 16 jela.

Waziri huyo, Maria Helena Taipo (60), amepatikana na hatia ya kufisidi fedha za umma ambazo zilipangwa kutekeleza baadhi ya miradi. Ni mwanachama wa chama tawala cha Frelimo.

Ilielezwa kuwa waziri huyo aliyedumu kwa miaka tisa katika wizara hiyo (2005 hadi 2014), alishtakiwa kwa ubadhirifu wa Sh. bilioni nne.

Hadi sasa mawaziri na viongozi wengine waandamizi wanane wa nchi hiyo wamefungwa kwa makosa ya rushwa. Hukumu zao zinaanzia miaka sita hadi 12.



*Maria Helena Taipo (60)*

# Ruto alaumu Idara ya Usalama

**Na Mwandishi Wetu, Nairobi**

ZIKIWA zimesalia siku nane kabla ya Wakenya kuamua nani awe rais wao, mgombea mmoja wa kiti hicho ameanza kunusa "mchezo mchafu" anaodai unafanywa na Idara ya Ujasusi ya Kenya.

Mgombea huyo, ambaye ni Naibu wa Rais, William Ruto anasema idara hiyo inaonekana kufanya kazi kwa kumpendelea mgombea mwenzake, Raila Odinga.

Kufuatia tuhuma hizo, Ruto anamtaka Rais Uhuru Kenyatta ambaye anamaliza muda wake, kuhakikisha idara hiyo haitumiki kuvuruga uchaguzi wa Kenya. Uchaguzi huo utafanyika Agosti 9, 2022.

Ruto amekuwa akirudia tuhuma hizo kwa idara inayopaswa kutopendelea mgombea yeyote kwenye uchaguzi huo na kuacha wananchi wenyewe kuamua wanamtaka nani kuongoza.

Anadai kuwa maafisa wa idara hiyo wameonekana wakiingilia hata maandalizi yanayofanywa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC).

Kiongozi huyo wa ushirika wa vyama wa Kenya Kwanza anadai serikali inatumia maafisa wa usalama kuvuruga maandalizi ya uchaguzi kwa lengo la kumsaidia mpinzani wake mkuu, Raila Odinga wa Azimio la Umoja - One Kenya.

"Nampa angalizo Rais Kenyatta kwamba hata kama yeye ni mwenyekiti wa Azimio, ni wajibu wake kufanikisha uchaguzi wa haki, ni vyema Rais Kenyatta akazuia idara kutumika kuvuruga uchaguzi. Asikubali kamwe kuacha nchi ikaharibika mikononi mwake," alisema Dkt. Ruto hivi karibuni alipokuwa akiendesha kampeni huko Kajiado.

Alionya kuwa kuna hatari ya kuahirishwa kwa uchaguzi iwapo maafisa wa idara wataendelea kuhangaisha tume ya IEBC.

Ruto alidai kuwa kuna ushirikiano mbaya kati ya serikali na viongozi wa Azimio kuipiga vita IEBC na mwenyekiti wa tume hiyo, Wafula Chebukati, "baada



*Mgombea urais wa Kenya, William Ruto*

yao kugundua kuwa watapoteza uchaguzi wa Agosti 9."

"Washindani wetu wamegundua kuwa tutawashinda. Hii ndio maana wameanzisha vita na IEBC ili uchaguzi uahirishwe. Wakenya wako tayari kwa uchaguzi. Wapinzani wetu wajue hawashindani na IEBC, bali wanashinda na sisi," Dkt. Ruto.

Naibu huyo wa Rais wa Kenya ameasa idara hiyo kuacha kuingialia masuala ya uchaguzi kwa kusaidia mpinzani wake kwa kuwa inajiharibia sifa na kwamba pamoja na kumsaidia mpinzani wake mkubwa, hawezi kumshinda kwani "tayari Wakenya wameamua yeye aongoze"

Hivi karibuni, idara hiyo ya ujasusi (usalama wa taifa) ilikamata watu watatu, akiwemo raia wa Venezuela, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA) wakiwa na kile kilichodaiwa kuwa ni "vifaa vya kuvuruga uchaguzi," kumsaidia Ruto.

Wengine waliokamatwa ni maofisa wa kitengo cha teknolojia cha IEBC. Hata hivyo, tume hiyo ilikanusha kuwepo kwa njama za kuvuruga uchaguzi.

**Zimebaki siku 7 Wakenya kuamua**

# Mtu, watu ni nani?

**Na Askofu Dkt. Stephen Munga**

KATIKA toleo lililopita nilizungumza juu ya magurudumu matatu yanayohitajika ili kuendelea kulingana na kauli za wahenga wa siasa Tanzania.

Magurudumu hayo yaliyotajwa mara kwa mara na Mwalimu Julius Nyerere (sasa marehemu); ni watu, siasa safi na uongozi bora. Kama nilivyosema naamsha mjadala huu ili kuona kama bado fikra zile zina maana kwa wakati wetu. Hii tutaiangalia kama falsafa nzuri ya maisha ya kijamii na kisiasa tunayokumbushana, lakini wakati huohuo kutumia ufafanuzi ninaofanya kama njia ya kukumbushana ikiwa ungalipo umuhimu huo. Leo nitaangalia dhana au gurudumu lile la watu. Mtu ni nani na watu ni nani?

Siku moja nikiwa kwenye mkutano mjini Moshi, Tanzania uliohusu masuala ya Ushiriki Mpya katika Maendeleo ya Afrika (NEPAD -New Partnership for Africa's Development). Ni wakati NEPAD ilipokuwa ikirindima kama njia yenye matumaini katika kuieletea Afrika maendeleo. Lengo langu hapa siyo kujadili NEPAD, bali kuleta mfano unaohusiana na hoja ya leo.

Ndani ya mkutano, wakati tunajadili juu ya maendeleo ya watu wa Afrika, aliamka mjumbe mmoja akauliza swali ambalo lilionekana kama vile hapakuwa na sababu ya msingi wa kuliuliza. Muuliza swali aliuliza swali rahisi tu, "watu ni nani?" Baada ya miguno mizito mjumbe mmoja akajibu kama kwa kebehi akisema, "watu ni watu."

Kukawa na kicheko na watu wengine waliendelea kuzoza wakidai kuwa wanapotezewa muda kwa maswali yasiyo ya msingi. Kwa kuona hali ya hewa ilivyokuwa, yule muuliza swali akaamua kunyamaza kimya.

Mara nyingi tunachukulia mambo kwa urahisi. Ni vyema kukumbuka kuwa kuna mambo makubwa katika maswali rahisi. Vumbuzi kubwa zimesimama katika maswali rahisi na Biblia inatukumbusha



*Hayati Baba wa taifa Julius Nyerere*

kuwa yeyote aliye mwaminifu katika mambo madogo, atakuwa mwaminifu kwenye mambo makubwa.

Katika magurudumu yale matatu ya maendeleo, swali hilo kuwa mtu/watu ni nani lisipojibiwa ipasavyo au kwa makosa, basi kwa hakika hata gurudumu la siasa safi na la uongozi bora yatakwenda kombo tu.

Kutokuliuliza swali hilo na kulipa nafasi ya tafakuri ya kina ni sawa na kujikimbia mwenyewe na kuonyesha wazi kwamba siyo muwajibikaji kwa nafsi yako na kwa wengine. Kutokulijibu swali hilo ipasavyo ndio chanzo cha kutengeneza watu wanafiki na wabinafsi wanaoishi kwa gharama za utu wa wengine.

Hatuwezi kueleza 'utu' ni nini kabla hatujajibu swali juu ya 'mtu' ni nani.

Swali lile pamoja na itikio lake vilionyesha mtazamo wa jamii yetu kwa ujumla. Kwamba watu walio wengi hawapendi kujishughulisha kujua mambo kwa undani. Hawapendi kujua hata juu yao wenyewe.

Pasipo kulijibu swali hili kwa usahihi hatuwezi kuyajibu maswali mengine yote kwa usahihi juu ya maisha yetu. Kwa hiyo kuanzia toleo lijalo nitalijibu swali hilo ili kuleta mwanga mpya katika namna ya kujitathmini.



## *Mezani kwa Chahali*

**Na Evarist Chahali**
evarist@chahali.com

# Rais Samia apanue wigo wa uteuzi

MOJA ya matukio yaliyotawala anga za habari nchini Tanzania ni mabadiliko yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika safu za wakuu wa mikoa.

Katika mabadiliko hayo, Rais Samia ameteua wakuu wa mikoa wapya tisa, amewahamisha vituo vya kazi saba, na kuwabakisha 10 katika vituo vyao vya kazi. Kadhalika, mkuu huyo wa nchi "amewatema" waliokuwa wakuu wa mikoa tisa.

Mabadiliko hayo yamepokewa kwa hisia tofauti, hususan miongoni mwa Watanzania waliojadili kwenye mitandao ya kijamii.

Kwa kiasi kikubwa, wengi wao walionekana kufurahishwa na uamuzi wa Rais Samia "kumtema" Ally Hapi, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara. Inaelezwa kuwa baadhi ya kauli za mwanasiasa huyo kijana zimekuwa zikiwakera watu mbalimbali.

Lakini, uteuzi ulioonekana kushangaza watu wengi ni wa Albert Chalamila kupewa tena mkoa, mwanasiasa ambaye kuna nyakati alionekana kama mwenye ucheshi uliopitiliza, huku akitoa kauli zisizoendana na hadhi yake.

Ni katika mazingira hayo, haikushangaza alipotolewa madarakani na Rais Samia, mwezi Juni mwaka jana. Baadhi ya watu wanajiuliza, "imekuwaje kuteuliwa tena katika nafasi ileile japo kituo kingine"?

Kwanza, ni muhimu kutambua na kuheshimu ukweli kwamba Rais ana mamlaka ya kumteua mtu yeyote yule anayeona anafaa kushika nafasi husika. Kwa hiyo, japo inaweza kushangaza watu, mamlaka yanamruhusu Rais Samia kumteua Chalamila.

Uteuzi wa Chalamila umeibua mjadala mpana zaidi kuhusu kada ya uongozi nchini Tanzania, hususan katika nafasi za kuteuliwa.




*Albert Chalamila*

Wengi wa walioteuliwa katika mabadiliko hayo ni wanasiasa ambao wamekuwa kwenye uongozi "miaka nenda miaka rudi." Licha ya ukweli kwamba hakuna sheria inayozuia mtu aliyewahi kuwepo kwenye uongozi kwa muda mrefu kuteuliwa tena, hoja ya kutetea inaweza kuwa pengine wateuliwa hao ni wachapakazi mno kiasi kwamba hakuna "mbadala wao."

Hata hivyo, kwa upande mwingine, taswira inayopatikana siyo tu kwenye baadhi ya teuzi hizo, bali pia katika sehemu kubwa ya uongozi wa taifa letu ni kana kwamba uongozi ni kwa ajili ya kundi fulani tu.

Pengine isingekuwa tatizo endapo uwepo kwenye uongozi kwa muda mrefu ungesaidia kuleta ufanisi mkubwa. Kwa bahati mbaya, baadhi ya watendaji "hufanya kazi kwa uzoefu" badala ya kuendana na mabadiliko mbalimbali.

Hivi karibuni nilimsikia naibu waziri mmoja akisema "Rais anachukizwa na kushuka kwa maadili." Nikajiuliza, kwahiyo laiti Rais asingechukizwa, naibu waziri asingeona kuwa hilo ni tatizo?

Nihitimishe kwa kutoa wito wa mamlaka za uteuzi kupanua wigo katika teuzi mbalimbali ili pia isaidie kuleta uwezo na akili mpya. Hata hivyo, sina tatizo na "sura zilezile miaka nenda miaka rudi" alimradi zinawatumikia Watanzania ipasavyo.

# Balozi wa Marekani anayependa 'kujichanganya'

**Na Tryruckia Mfinanga**

DAKTARI Donald Wright akiwa na muda, utamkuta kila mahali; anakuwa vijiweni akipiga soga na vijana; akiwa kwa washona viatu; akiwa kwa mama ntilie - akila ugali kwa samaki na mlenda; akiwa kwa wauza chipsi na maeneo mengine ya kawaida Dar es Salaam na mikaoni.

Huyu ni Balozi wa Marekani nchini Tanzania. Ni mtu mkubwa. Ni mwakilishi wa taifa lenye nguvu imara ya uchumi na nguvu kubwa ya kijeshi.

Kwa hadhi na mzingira yake na dhamana anayoshikilia, alitarajiwa kuwa kiongozi anayejitenga na watu wa kawaida. Anayezungukwa na wazungu wenzake na kuonekana kwa nadra akiwa na viongozi wa Tanzania, hasa rais, makamu na pengine waziri mkuu.

Lakini, Dkt. Wright kwake ni tofauti. Anapenda kujichanganya akisalimiana na watu wa kawaida mitaani, akisogoa na hata kuonekana akila na kunywa nao. Ni balozi tofauti na waliozoeleka, wanaokuja kuwakilisha nchi zao hapa Tanzania.

Wauza madafu na mihogo, eneo la Ufukwe wa Coco, Dar es Salaam, ni marafiki wakubwa wa Balozi Wright na hupenda kumkaribia na kuzungumza naye kila wikiendi anapowatembelea wakati akifanya matembezi.

Mmoja wa wauza mihogo katika banda maarufu la ITV, Mika Banda, anasema balozi wa Marekani ni rafiki mkubwa wa watu wa eneo hilo, na kwamba kila anapokuja hununua mihogo na kunywa madafu.

Balozi Wright anakiri kwamba anapenda kunywa maji ya madafu kwa sababu ni mazuri kwa afya na kwamba hupenda 'kuwaunga' mkono vijana wanaofanya kazi zao eneo hilo na maeneo mengine.



*DAKTARI Donald Wright akila nyama choma Mkoani Arusha maeneo ya Kwa Morombo*

# Balozi wa Marekani anayependa ‘kujichanganya’

“Napenda sana kunywa maji ya madafu na kuzungumza na marafiki zangu wa eneo hili, ni watu wazuri sana, wanajibidiisha kwa kufanya kazi halali,” anasema balozi huyo.

Ni kutokana na ukaribu huo wa ‘kujichanganya’ na watu wa kawaida, Dkt. Wright anawajua vyema wapishi maarufu wa chapati, mafundi viatu maarufu na anatambua sehemu anakoweza kupata samaki sato wakubwa na ‘fresh’ kutoka Mwanza.

Balozi Wright anamtambua Mama Miraji, mama ntilie anayefanya biashara yake ya kuuza chakula maeneo ya Msasani, Jijini Dar es Salaam.

“Namshukuru sana Balozi wa Marekani kuja kuniunga mkono kwenye biashara yangu ya kuuza chakula, wala sikuamini kama siku moja naweza kutembelewa na mtu mkubwa kama yeye na kula kwa mama ntilie,” anasema Mama Miraji.

Mwantumu Maezi, mchuuzi wa mahindi ya kuchoma eneo la Kihesa, Iringa ambako Balozi Wright aliwahi kusimama na kununua mahindi kutoka kwake anasema, “sijawahi kuona mzungu, tena naambiwa ni balozi, anakuja kununua mahindi, tena bila kulalamika kupunguziwa bei.”

Anapokuwa Iringa, Balozi Wright hupendelea kufika, kufanya maongezi na kula ama kunywa kahawa na walemavu, hasa wanaoendesha mgahawa maarufu mjini humo – Neema Craft. Wahudumu wote wa mgahawa huo ni walemavu.

Balozi Wright alifika Tanzania na kuanza majukumu ya ubalozi mwaka 2020, huku akieleza kwamba atajikita katika maeneo kadhaa ya muhimu ya kufanya kazi ili kuboresha maisha ya Watanzania. Alitaja maeneo hayo kuwa ni maisha ya watu, afya, elimu na biashara.

Akiwa daktari wa magonjwa ya binadamu, Balozi Wright haikuwa mara yake ya kwanza kufika na kufanya kazi Tanzania. Mara ya kwanza alifika miaka 30 iliyopita, akiletwa kufanya kazi ya udaktari katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Zanzibar, ambako alihudumu zaidi kwa kutibu watoto.

“Nilipofika mara ya kwanza Tanzania, na hasa Zanzibar, nilivutiwa mno na ukarimu wa watu wake na namna walivyokuwa wakishirikiana nami na wenzangu kufanya kazi za kitabibu, hivyo nilipopata taarifa ya kurudi nikiwa balozi, nilifurahi sana,” anasema.

Dkt. Wright pia hutumia zaidi mitandao ya kijamii, hasa Twitter, ambako huweka taarifa mbalimbali, zikiwamo za kikazi na maisha yake binafsi.

Katika ukurasa wake wa Twitter ambako anawatu 45,600 wanaomfuatilia, huku yeye akiwafuata watu 32 tu. Miongoni mwao ni pamoja na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi; Waziri wa Habari, Nape Nnauye; Balozi wa Tanzania nchini Marekani, Elsie Kanza na Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe. Wengine ni mabalozi na mashirika ya kimataifa.



*Balozi Wright akifurahia muhindi wake.*

# Tanzania iamue kuwa tajiri

**Na Godwin Chilewa, Texas, Marekani**

KILA Jimbo la Marekani kuna vivutio lukuki vinavyosaidia kuingizia mapato serikalini; kila ziwa, kila mto, kila bonde la kupendeza au msitu, ni chanzo cha mapato.

Viko vituo vya makumbusho ya kila kitu; kuanzia vifaa vya anga, bahari, sayansi, sanaa, jeshi na silaha zake (manowari, vifaru na mizinga) na hata ujasusi (Spy Museum). Hivi vyote ni vyanzo vya mapato.

Mapato haya, yakichanganywa na kodi mbalimbali zinazokusanywa, huiwezesha serikali kugharimia miradi mikubwa na kuondoa tozo lukuki kila mahali. Kwa mfano, serikali hutoa kompyuta mpakato bure kwa wanafunzi wote wa shule za msingi na sekondari.

Nimeelezea haya yote ili kuonesha haja ya Serikali ya Tanzania kufikiria na kubuni vyanzo vipya vya mapato, badala ya kuwatoza wananchi maskini fedha kidogo walizonazo kwenye miamala ya simu.

Tanzania inavyo vivutio vingi ambavyo kama vikihuishwa vinaweza kutoa ajira kwa wananchi na kuwafanya wao wazirudishe serikalini kwa furaha kupitia matumizi yao. Wananchi wa Tanzania ni watumiaji wazuri sana wa fedha, na kama huamini angalia idadi ya watu waliotembelea Viwanja vya Maonyesho ya Sabasaba kila mwaka na wale wanaohudhuria viwanja vya mpira kuangalia soka.

Kama watu wanaweza kutembelea mabanda ya Sabasaba, siyo ajabu kuwa wanaweza kutembelea vivutio vingine vya ndani kama vikijengwa na wakihamasishwa kufanya hivyo. Leo hii mtu akitembelea jijini Dar es Salaam, hana sehemu nyingi za kutembelea kwa kujifunza. Zamani kila mtu alikwenda soko la Kariakoo maana lilionekana ndiyo muujiza. Leo hii limekuwa kitu cha kawaida sana.

Ndiyo maana najiuliza, kwa nini jeshi la Wananchi wa Tanzania hawafungui eneo kubwa la makumbusho jijini Dar es Salaam kuonesha silaha mbalimbali zilizotumika kumng’oa nduli Iddi Amini. Nina hakika huo ungekuwa mradi mkubwa wa kuliingizia mapato jeshi, kuwafundisha vijana wetu historia, na kuwajaza uzalendo na kiu ya kulitumikia Taifa kwa dhati.

Au kwa nini chuo kikuu cha sayansi na Tiba Muhimbili hakijengi makumbusho ya sayansi na tiba kwa ajili ya kuwaonesha vijana na wazee wetu mfumo wa mwili wa binadamu ulivyo, na kuelekeza jinsi madaktari wanavyotumia sayansi katika kuokoa maisha ya watu?

Haya ndiyo huwa wanayaonesha kwenye mabanda ya Sabasaba? kwa nini kisijengwe kituo ambapo wanafunzi wanaotamani kuwa madaktari kutoka kila kona ya Tanzania, wanaweza kutembelea kwa kulipa kiasi fulani cha pesa? Tunashindwa nini? Mbona wenzetu wanafanya na wanaingiza pesa?

***Itaendelea wiki ijayo...***

# Neema ya umeme wa uhakika yaja Z'Bar



*Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hussein Mwinyi.*

**Na Jabir Idrissa, Unguja**

BENKI ya Dunia imekubali kuipatia mkopo wa masharti nafuu Serikali ya Zanzibar wa Dola 142 milioni kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kurekebisha sekta ya uzalishaji wa nishati ya umeme.

Taarifa za ndani ya Benki hiyo zimeeleza kuwa mkopo huo utawezesha serikali kujihakikishia upatikanaji wa uhakika wa umeme kutokana na matarajio ya mageuzi makubwa ya mfumo wa uzalishaji wa umeme.

Kwa mujibu wa taarifa hizo, utekelezaji wa mradi huo utahusisha ujenzi wa mtandao mpya wa miundombinu wa kuwezesha kupatikana umeme wa uhakika.

Mradi huo unaotambulika kama ZESTA - Urekebishaji wa Mfumo wa Umeme na Uhakika wa Upatikanaji – ambao unatarajiwa kukamilika mwaka 2026. Mradi utaiondoa Zanzibar kutegemea kwa kiasi kikubwa umeme kutoka Tanzania Bara.

Pambazuko limeelezwa hivi karibuni na maofisa waandamizi katika Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Zanzibar kuwa utekelezaji mradi utahusu ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha nishati jadidifu; kuboresha Gridi ya Taifa kuwa wa mfumo wa Kilovoti 132 badala ya Kilovoti 32 uliopo kwa miaka yote ambayo Zanzibar imekuwa ikitegemea nishati hiyo kutoka Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco); na kwamba taratibu zinaendelea kuwezesha kushiriki kwa wawekezaji binafsi.

Ushiriki wa wawekezaji unatarajiwa kufanikisha ongezeko la umeme wa jua upatao Megawati 18. Uzalishaji huo utafanyika kijiji cha Makunduchi, Wilaya ya Kusini Unguja, kuzingatia utafiti uliofanywa kwa ushirikiano wa serikali na wataalam wa Umoja wa Ulaya - European Union (EU).

Maofisa hao wameeleza matumaini yao kuwa kufanikiwa kwa mradi huo unaotekelezwa kwenye mikoa yote mitatu ya kisiwa cha Unguja - Mjini Magharibi, Kaskazini na Kusini - kutakuwa na manufaa makubwa kwa vile "kutapunguza tatizo sugu la kukatika kwa umeme na kuzorota kwa usafirishaji umeme kutumia nyaya za baharini kutokana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi."

"Kukamilika kwa mradi huu itakuwa mwanzo wa safari ndefu ya Zanzibar kuwa na chanzo chake cha umeme badala ya kutegemea umeme unaozalishwa na Tanesco. Pia itakuwa ni fursa kwa uwekezaji binafsi wa sekta ya nishati ya umeme," anasema Dkt. Mngereza Miraji Mzee aliyeshiriki majadiliano ya awali kabisa yaliyowezesha mradi kukubaliwa na Benki ya Dunia.

Tangu mwaka 1978 Zanzibar ambayo shirika lake la umeme - ZECO - ndilo pekee linalotoa huduma ya uzalishaji na usambazaji wa umeme kwa wateja, imekuwa ikinunua umeme kutoka Tanesco.

# Tutakumbuka Daima...



*KWAMBA Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitembelea Ethiopia na kupokewa na mwenyeji wake, Mfalme Haile Selassie wa nchi hiyo. Hii ilikuwa Novemba 4, 1966. Katika picha hii, Mwalimu (kushoto) akiwa na Mfalme Selassie katika Uwanja wa Ndege wa Addis Ababa, Mji Mkuu wa Ethiopia. Katika ziara hiyo, Mwalimu Nyerere pia alihudhuria kikao cha Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU). Viongozi wote hawa ni marehemu. (Picha na Maktaba ya Pambazuko).*

# Kujitambulisha




**Na Dkt. Michael Mashauri**

KISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Leo Mwalimu anazungumzia juu ya namna nzuri na sahihi ya kujitambulisha (introducing yourself).

Kabla ya kujifunza namna ya kujitambulisha, tujifunze kwanza viwakilishi vya nafsi vya Kiswahili (Before learning how to introduce oneself; we should first learn Swahili personal pronouns).

| **Umoja (Singular)** | **Wingi (Plural)** |
|---|---|
| 1st Person Mimi (I/me) | sisi (we/us) |
| 2nd person Wewe (you) | ninyi/nyinyi (you all) |
| 3rd person Yeye (he/she or him/her) | wao(they/them) |

**Kila kiwakilishi cha nafsi huwa na kipatanisho kiima chake katika vitenzi (Every personal pronoun has its grammatical subject concord in the verb).**

**Examples**:

Mimi (ni-) sisi (tu-)
Wewe (u-) nyinyi (m-)
Yeye (a-) wao (wa-)

**Namna ya Kujitambulisha (How to introduce yourself)**

**Hawa:** Habari gani kaka? (How are you brother)
**Masanja:** Nzuri kabisa (absolutely fine)
**Hawa:** Mimi ninaitwa Hawa, wewe je?(I'm called Hawa, what about you?)
**Masanja:** Mimi ninaitwa Masanja (I am called Masanja)
**Hawa:** Ninafurahi kukufahamu
**Masanja:** (I am happy to know you Masanja)
**Masanja:** Asante Hawa (Thank you Hawa)
**Hawa:** Kwa heri Masanja (Goodbye Masanja)
**Masanja:** Haya, kwa heri Hawa (Okay, Goodbye Hawa)

**Ifuatayo ni namna nyingine ya kujitambulisha (The following is the other way of introducing oneself).**

**Baraka:** Habari za asubuhi! (Good morning)
**Furaha:** Nzuri, wewe je hujambo? (Good morning/fine, what about you?)
**Baraka:** Mimi pia sijambo, Jina langu ni Baraka, jina lako (ni) nani? (I am also okay, My name is Baraka, what is your name?)
**Furaha:** Jina langu ni Furaha (My name is Furaha)
**Baraka:** Unatoka wapi Furaha? (Where are you FromFuraha?)
**Furaha:**Mimi ninatoka Ghana (I am from Ghana)
**Baraka:** Unakaa wapi? (Where do you stay?)
**Furaha:** Sasa mimi ninakaa Mwenge (I am now staying at Mwenge)
**Baraka:** Unafanya kazi gani? (What is your occupation?)
**Furaha:** Mimi ni mwanafunzi, wewe je? (I am a student, what about you?)
**Baraka:**Mimi ni mfanyabiashara (I am a businessman)
**Furaha:**Haya, kwa heri (Okay, goodbye)
**Baraka:** Kwa heri Furaha (Goodbye Furaha)

• ***Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.***

# Ujue mradi wa reli ya kisasa

**Na Mwandishi Maalum**

RELI ya kati kwa kiwango cha kisasa ni mfumo wa reli unaojengwa ambao unaunganisha Tanzania na nchi jirani za Rwanda, Uganda, Burundi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

**Malengo**

Malengo ya mradi ni kupunguza gharama za usafiri, kupunguza muda wa kusafiri, ufikiaji rahisi kwa huduma mbalimbali za jamii kwa jumuiya ya eneo la mradi na uwezeshaji wa biashara kati ya Tanzania na nchi za jirani.

Njia hii ya reli yenye jumla ya 1,435 (4 ft 8 1/2 in) inalenga kurahisisha usafiri wa bidhaa kati ya bandari ya Dar es Salaam na miji ya Kigali, nchini Rwanda na baadaye Bujumbura, Burundi, na Goma, katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kutoka bandari ya ziwa Victoria katika Jiji la Mwanza, feri zinatarajiwa kusafirisha bidhaa kati ya Mwanza na Port Bell na Port Bukasa, Kampala, mji mkuu wa Uganda. Reli hii ya SGR inatarajiwa kutumiwa na treni za abiria ambayo inatarajiwa kusafiri kilomita 160 (99 miili) kwa saa na treni za mizigo kusafiri kilomita 120 (75 mi) kwa saa.

**Ujenzi wa Reli na Maeneo itakayopitia**

Mradi ulianza mnamo mwezi Aprili 2017 ambapo awamu ya kwanza, ujenzi ulianzia Dar es Salaam mpaka Morogoro kwa umbali wa Kilometa 300 (maili 186). Reli hiyo inaanzia katika bandari ya Bahari ya Hindi, Dar es Salaam hadi katika pwani ya Mwanza kwenye Ziwa Victoria ili kuunganisha nchi jirani.

**Reli inapitia katika maeneo yafuatayo:** Dar es Salaam, Morogoro, Makutopora (Dodoma), Tabora, Isaka (Shinyanga), Mwanza, Rusumo (Kigali,Rwanda), Bujumbura (Burundi), Goma (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) na Kampala (Uganda).

**Hatua za Ujenzi**



**Mfumo wa reli una sehemu kadhaa kuu:**

Sehemu ya Dar es Salaam – Morogoro: Sehemu hii ina kilomita 300 (186 mi), Ujenzi ulianza Aprili 2017, na unaendelea kwa kujenga nguzo pamoja na kuweka mataluma.

Sehemu ya Morogoro-Dodoma: Kuanzia Morogoro kwenda Makutupora, mji mkuu Dodoma, una urefu wa kilomita 426 (265 mi).

Sehemu ya Dodoma-Isaka: Sehemu hii ina umbali wa kilomita 435 (270 mi), kutoka Makutupora, Dodoma, hadi Isaka, Tabora

Sehemu ya Isaka-Mwanza: Sehemu hii ina umbali wa takriban kilomita 220 (137 mi), inapitia jiji la Mwanza, kwenye mwambao wa kusini mwa Ziwa Victoria.

Sehemu ya Isaka-Rusumo: Hii ni sehemu ya Reli ya Kigali, ina umbali wa kilomita 371 (231 mi).

**Fursa**

Kuna nafasi za kazi kwa wahandisi, wafanyakazi wa kawaida na madereva na pia biashara kama vile za Mama Lishe, wafanyabiashara wadogowadogo (Marching Guys), bidhaa za viwandani n.k . Wahandisi na madereva wanapaswa kujiandikisha ili kupata fursa hizo pamoja na wafanyakazi wa kawaida wanapaswa kufikia eneo husika la mradi ili kupata fursa.

***- Imetolewa kwenye wavuti ya miradi ya serikali***

# Concorde yapata mbadala



WASAFIRI wa ndege sasa kutumia muda mfupi zaidi wanaposafiri kutoka eneo moja hadi jingine baada ya wataalamu kugundua ndege iliyopewa jina la Boom.

Ndege hiyo ambayo inatarajiwa kuanza safari zake mwaka 2026, itakuwa na kasi zaidi ya ndege nyingine aina ya Concorde.

Boom, itasafiri kwa kasi mara mbili na nusu zaidi ya ndege za kawaida kufikia mwendo wa maili 1,451 sawa na kilomita 2,335 kwa saa. Concorde ilikuwa ikisafiri kwa kasi ya maili 1,350 sawa kilomita 2,170 kwa saa.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa wanasayansi, ndege hiyo itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 40 kwenye mistari miwili na itawawezesha abiria wanaosafiri kutoka London kwenda New York Marekani kufika chini ya muda wa saa tatu na nusu. Ticket moja itagharimu Dola za Kimarekani 5,000 sawa na shilingi za Kitanzania milioni 11,518,000.

“Tunazungumzia ndege ya kwanza yenye mwendo kasi zaidi duniani ambayo watu wanaweza kumudu gharama zake,” mgunduzi wa ndege hiyo na Ofisa Mtendaji Mkuu Blake Scholl aliliambia gazeti la Guardin la Uingereza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Boom, Blake Scholl anasema vifaa vya kutengeneza ndege hiyo havitakuwa na uzito mkubwa, hivyo kuiwezesha ndege hiyo kuwa na mwendo kasi kuliko ndege zote duniani.

Ndege hiyo bado ipo kwenye hatua za mwisho za matengenezo lakini lengo la kampuni ya Scholl ni kujaribu ndege ya kwanza mwishoni mwa mwaka huu katika mji wa Colarado.

Timu ya marubani, wahandisi wa ndege pamoja na wajenzi wanaohusika na ugunduzi wa ndege hiyo ya abiria, wameunda kampuni sita na watashiriki katika utengenezaji wa ndege 30.

Kampuni hiyo ilipata kuungwa mkono na kampuni ya Richard Branson’s Virgin Group, ambayo ipo kwenye mchakato wa kutengeneza ndege ya abiria itakuyoruka anga za mbali.


Scholl anasema ndege hiyo itaweza kuziba nafasi ya Concorde ambayo ilishindwa kujiendesha kutokana na gharama za nauli kuwa kubwa.

“Ni vigumu kuweza kupata abiria wa kutosha kwa gharama ya Dola za Marekani 20,000 kwa abiria mmoja, hii ndiyo sababu iliyowafanya Concorde kushindwa kuendelea kuwapo,” anasema Scholl.

Anaongeza; “tutakachofanya ni kupunguza bei ya tiketi na kufanya ndege kuwa na umbo la kawaida ili kutuwezesha kuruka kwa mwendo kasi zaidi.”

***Makala haya yametolewa vyanzo mbalimbali***

# Shikeni mimba mapema- Daktari



*Mtoto anavyoonekana akiwa tumboni*

**Na Tryruckia Mfinanga**

SAYANSI inayohusika na mabadiliko ya mwili wa binadamu, inaeleza kwamba uwezekano wa mwanamke kushika mimba akiwa na umri kuanzia miaka 35 na kuendelea, hupungua.

Sambamba na ukweli huo, pia uwezo wa mwanaume akiwa na umri wa miaka 40 na kuendelea – kutungisha mimba, hupungua kwa kiasi kikubwa.

Pamoja na ukweli huo, lakini bado wapo wanawake wenye uwezo wa kushika mimba na wanaume wenye kutungisha, wakiwa na umri mkubwa zaidi ya huu unaotajwa na kuthibitika kisayansi.

Umri mzuri unaotajwa na sayansi wa kushika na kutunga mimba ni kuanzia miaka 20 na kuendelea hadi miaka 30 -kwa wanawake na wanaume. Ni katika umri huu, mimba inapotungwa, uwezekano wa kupatikana kwa mtoto mwenye afya ni mkubwa zaidi kuliko wale wenye umri mkubwa.

Katika nyakati hizi ambazo zinatawaliwa na elimu na utambuzi wa mambo mengi, wanawake – hasa wa mijini wamekuwa na tabia ya "kujipanga" kwanza kabla ya kupata mtoto.

Wengi wao hutamani kuwa na maisha bora kwanza ndipo wapate watoto, wakiwa na maana ya kuwa na nyumba, gari na kipato kikubwa kwa madai ya kuwa na uwezo mkubwa wa kuleta mimba na hata mtoto.

Daktari bingwa wa via vya uzazi kutoka Dar es Salaam, Tanzania, Eliakim Maswila,anaeleza kuwa ni vyema kwa wanawake kupata watoto wakiwa bado via vyao vya uzazi havijachoka kutokana na umri.

Anaeleza kwamba binadamu viungo vyake vya mwili – ikiwamo via vya uzazi, huanza kuchoka kadri umri unavyoongezeka, hivyo kabla havijafikia kupunguza uwezo wake wa kufanya kazi vyema, ni vizuri wanawake wakapata watoto bila kujali uwezo wao wa kiuchumi.

"Ukipata watoto mapema, afya ya mama inakuwa salama na afya ya watoto pia, lakini ukichelewa, madhara yanaweza kuwa makubwa kinyume na matarajio," anaongeza mtaalamu huyo.

Daktari huyo anaeleza kuwa kulingana na wataalamu, mwanamke huzaliwa na mayai ya uzazi ya kutosha, lakini huenda yakipungua nguvu kadri umri unavyosonga, "hivyo kushika mimba mapema ni jambo la busara."

Wakati ambapo ni rahisi kushika mimba ni ukiwa chini ya umri wa miaka 30. Kwa upande mwingine uwezo wa kushika mimba huanza kupungua ukitimu umri wa miaka 35 na hata zaidi.

Lakini pia uwezo wa wanaume kutungisha mimba huanza kupungua wakishatimu miaka 40, na umri wa mwanamume huathiri uwezekano wa mwanamke kushika mimba, iwe kwa njia ya kawaida au kupitia ya kupandikiza - In Vitro Fertilization (IVF).

# Mdomo wa Mandonga zaidi ya ngumi zake

**Na Mwandishi Wetu**

INAELEZWA na wataalamu wa ndondi kwamba bondia kuwa na tambo kabla ya pambano ni jambo la kawaida, lakini wapo wanaotamba na kupitiliza.

Miongoni mwa hao wanaotamba na kupitiliza ni bondia wa Tanzania, Karim Mandonga ambaye kabla ya pambano lake na Shaaban Kaoneka - Julai 30, 2022



***Karim Mandonga***

alisikika kila kona akitamba kwamba mpinzani wake "ajiandae kwenda kaburini."

Mandonga alikuwepo kwenye kila chombo cha habari, kuanzia redio, televisheni, mitandao ya kijamii, akitamba kwamba mpinzani wake aje akijua anakwenda kupoteza maisha, kwani hatarejea salama kwake.

"Huyu amezoea viazi, lakini sasa anakuja kupambana na mzizi wa muhogo, lazima atakaa chini na jamaa zake waje na jeneza, kwani anaenda kumaliza kazi kabisa, sitaki mchezo mimi," alisikika akitamba Mandonga.

Mpinzani wake, Kaoneka hakusikika kabisa akitamba, zaidi ya kueleza kwamba anajua anachoenda kufanya na kwamba matokeo ndiyo yatamueleza yeye ni nani.

Katika mchezo huo uliofanyika Uwanja wa Majimaji, Songea ukiwa na raundi 12 - uzito wa juu, Mandonga alianza pambano kwa "kuruka-ruka" huku akijitahidi kukwepa ngumi za Kaoneka, ambaye alionekana akiwa mtulivu na 'kumsoma' Mandonga; namna anavyorusha ngumi na kukwepa zake.

Raundi ya tatu ilianza kuonyesha kuchoka kwa Mandonga baada ya kurushiwa ngumi kadhaa ambazo zilitua kwenye uso ama kidevuni kwakwe.

Kwa tathmini ya mchezo katika raundi tatu za mwanzo, Mandonga alikosa stamina na alionekana kama bondia asiyekuwa na maandalizi mazuri kabla ya pambano.

Raundi ya nne ilidhihirisha kwamba Mandonga amechoka, kwani kila ngumi iliyorushwa na Kaoneka, ilitua kwenye kichwa chake na alionekana 'kuvurugwa' – kwani tayari miguu yake ilitembea kwa kulegea.

"Sura yake ilibeba alama ya kumwambia mwamuzi asimamishe mchezo kwani alikuwa na hali mbaya na alizidiwa sana na ngumi za Kaoneka," alisikika shabiki mmoja.

Mwamuzi aliamua kusimamisha pambano raundi ya nne, baada ya kumuona Mandonga amechoka na kwamba asingeweza kumudu kuendelea na kichapo kutoka kwa Kaoneka.

Kusimamishwa kwa pambano hilo, kukawa mwokozi kwa Mandonga, kwani huenda angeumia zaidi kwa ngumi kutoka kwa mpinzani wake.

Baada ya mchezo, Mandonga alisema kupigwa kwake ni bahati mbaya sana na kwamba mchezo huo siyo rahisi kama kila mmoja anaweza kudhani.

Pia Mandonga akasema; "kushindwa kwake ni mipango ya Mungu, kwani yeye alipanga kumchakaza kabisa Kaoneka, lakini kumbe Mungu ana mipango yake."

Kwa pambano la Mandonga na Kaoneka, ni dhahiri kuwa ngumi za Mandonga ni nyepesi kuliko mdomo wake ambao unabeba maneno mazito mno, hivyo kuwa gumzo kila kona kabla ya mchezo.

# PICHA KUBWA

*Mwanariadha wa Tanzania, Alphonce Felix Simbu akiwa na furaha baada ya kutwaa medali ya Fedha kwa kuibuka mshindi wa pili kwenye mbio za marathon katika Michezo ya Jumuiya ya Madola jijini Birmingham, Uingereza – Julai 30, 2022. Simbu alitumia muda wa saa 2:13:16, nyuma ya Victor Kiplagat wa Uganda aliyekuwa mshindi kwa kutumia saa 2:10:55. (Picha na Mpigapicha Maalum).*




*GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION